

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



PROGRAMU YA MAENDELEO YA SEKTA YA ELIMU

MWONGOZO WA HESABU NA USIMAMIZI WA FEDHA

Imeidhinishwa na Kamati ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi
Marekebisho
April 2003

MWONGOZO WA MEMM WA HESABU NA USIMAMIZI WA FEDHA

**MWONGOZO WA HESABU NA USIMAMIZI WA FEDHA WA PROGRAMU YA
MAENDELEO YA SEKTA YA ELIMU**

**YALIYOMO
ORODHA YA AKRONIMI NA VIFUPISHO**

1	LENGO NA MADHUMUNI YA MWONGOZO	1
1.1	MALENGO.....	1
1.2	MADHUMUNI.....	1
1.3	MAJUKUMU KUHUSU TARATIBU ZILIZOMO KWENYE MWONGOZO.....	2
1.4	HATUA ZA NIDHAMU	2
2.	MUUNDO WA KITAASISI NA MAJUKUMU	2
2.1	KAMATI YA UENDESHAJI YA WIZARA ZINAZOONGOZA PEDP	2
2.2	KAMATI YA MAENDELEO YA ELIMU YA MSINGI (BEDC)	2
2.3	BENKI KUU YA TANZANIA	3
2.4	MHASIBU MKUU.....	3
2.5	OFISI YA RAISI-TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)	3
2.6	WIZARA YA ELIMU NA UTAMADUNI (MOEC).....	4
2.7	SEKRETARIATI ZA MIKOA	5
2.8	HALMASHAURI	5
2.9	KAMATI YA SHULE	6
3.	BAJETI NA MIPANGO	
3.1	MIPANGO KATIKA MoEC NA TAMISEMI	7
3.2	MIPANGO KATIKA NGAZI YA HALMASHAURI	7
3.3	BAJETI KATIKA MoEC YA MATUMZI YA MFUKO WA PROGRAMU YA ELIMU	8
3.4	BAJETI KATIKA NGAZI YA HALMASHAURI KWA AJILI YA MFUKO WA PROGRAMU YA ELIMU	10
3.5	RATIBA YA JUMLA YA BAJETI NA MIPANGO	14
4	ULIPAJI/UTOAJI WA FEDHA	
4.1	UENDESHAJI WA AKAUNTI YA PAMOJA YA MMEM	14
4.2	KUZIHAMISHIA KATIKA WIZARA/IDARA	17
4.3	KUZIHAMISHIA KATIKA HALMASHAURI/SHULE.....	18
5	SERA NA MIFUMO YA HESABU	
5.1	PROGRAMU YA SERA ZA HESABU	22
5.1.1	MAELEZO YA JUMLA	22
5.1.2	KANUNI ZA HESABU	22
5.1.3	MSINGI WA HESABU.....	22
5.1.4	MAPATO KWA AJILI YA PROGRAMU	22
5.1.5	MATUMIZI YATAKAYOGHARIMIWA NA PROGRAMU ...	22
5.1.6	RASILIMALI ZA KUDUMU NA VIFAA VYA KAWAIDA....	22
5.2	MIFUMO YA HESABU NA TARATIBU	23
5.2.1	AKAUNTI INAYOMILIKIWA KATIKA BENKI KUU YA	

MWONGOZO WA MEMM WA HESABU NA USIMAMIZI WA FEDHA

TANZANIA	23
5.2.2 MOEC NA WIZARA KUU	25
5.2.3 TARATIBU ZA MALIPO KWA HALMASHAURI	25
5.2.4 TARATIBU ZA MALIPO KATIKA NGAZI YA SHULE YA MSINGI	25
5.2.4.1 MAPATO.....	25
5.2.4.2 TARATIBU ZA MALIPO KWA SHULE	25
6 UNUNUZI NA USIMAMIZI WA RASILIMALI	
6.2.1 RASILIMALI ZA KUDUMU	27
6.2.2 RASILIMALI KATIKA KIWANGO CHA SHULE.....	28
6.2.3 REJISTA YA VITABU KATIKA NGAZI YA SHULE ...	28
7 RIPOTI ZA TAARIFA ZA USIMAMIZI	
7.1 MWELEKEO WA RIPOTI.	28
7.2 AINA YA RIPOTI ZILIZOTAYARISHWA	28
7.2.1 RIPOTI ZA WIZARA YA FEDHA	28
7.2.2 RIPOTI ZA MOEC/OFFISI YA RAIS-TAMISEMI KWA KUZINGATIA SHUGHULI KUU	29
7.2.3 RIPOTI ZA OFFISI YA RAIS-TAMISEMI KWA KUZINGATIA SHUGHULI ZA HALMASHAURI	30
7.2.4 HALMASHAURI.....	31
7.2.5 KAMATI YA SHULE.....	33
8 UKAGUZI WA NDANI NA NJE	
8.1 WIZARA KUU	33
8.2 HALMASHAURI	33
8.3 SHULE HUSIKA	33
9 VIAMBATISHO	
KIAMBATISHO A	35
KIAMBATISHO B	41
KIAMBATISHO C	56
KIAMBATISHO D	58
KIAMBATISHO E	62
KIAMBATISHO F	72
KIAMBATISHO G	81
KIAMBATISHO H	86

MWONGOZO WA MEMM WA HESABU NA USIMAMIZI WA FEDHA**Orodha ya vifupisho**

ACCGEN	Mhasibu Mkuu wa Serikali
BEDC	Kamati ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi
BoT	Benki Kuu ya Tanzania
CAG	Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali
CD	Mkurugenzi wa Halmashauri (Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya, Mkurugenzi wa Jiji/Manispaa/Mji)
CPO	Ofisi Kuu ya malipo
ESDP	Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu
CEO	Ofisa Elimu wa Halmashauri
IFMS	Mifumo ya Hesabu na usimamizi wa Fedha ya Uwiano.
IMSC	Kamati ya Uendeshaji ya Wizara zinazoongoza ESDP
LPO	Dhamana ya Ununuzi
MoEC	Wizara ya Elimu na Utamaduni
MoF	Wizara ya Fedha
NGO	Asasi zisizo za serikali
PEDP	Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi(MMEM)
POAB	Mpango wa utekelezaji na Bajeti
PS	Katibu Mkuu
RS	Sekretariati ya Mkoa
TAMISEMI	Ofisi ya Raisi-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

Kwa matumizi ya mwongozo huu shule inafasiriwa kama shule ya msingi inayofadhiliwa na serikali.

MWONGOZO WA MEMM WA HESABU NA USIMAMIZI WA FEDHA

1. LENGU NA MADHUMUNI YA MWONGOZO

1.1 Malengo

Malengo ya Mwongozo huu ni kuweka taratibu na sera za hesabu ambazo zinahitajika hasa kwa ajili ya kupanga na kusimamia fedha za MMEM.

Serikali ya Tanzania kwa kuwa ni mnufaika, itahakikisha kwamba mifumo mizuri ya utoaji taarifa na usimamizi wa fedha itatumika wakati wa kutumia rasilimali ilizotengewa. Mfumo wa fedha utashughulikia mahitaji ya utoaji taarifa ya wabia mbalimbali wanaoshiriki katika programu.

1.2 Madhumuni

Madhumuni ya mwongozo wa taratibu za fedha ni kuwawezesha wale watakaohusika na kazi za programu za kila siku kufanya kazi zao vizuri, kwa ufanisi na ubora, na wakati huo huo kuwapa taarifa muhimu kwa ajili ya utoaji mzuri wa maamuzi.

Mwongozo unakuwa kama kiongozi kwa kila mtu na taasisi zinazotekeleza shughuli za MMEM kuhusu taratibu za fedha ili kuwezesha kuundwa na kusimamiwa kwa mifumo mizuri ya usimamizi wa fedha ili kuwezesha taarifa za fedha kupatikana kwa wakati.

Mwongozo unatoa taarifa kuhusu mambo mbalimbali ya mipango ya utawala na usimamizi wa fedha. Unalenga katika kutimiza majukumu na uwajibikaji, taratibu za ulipaji, michakato ya hesabu, usimamizi wa rasilimali na utoaji wa taarifa. Aidha, unatoa miundo ya majedwali muhimu kwa masharti ya utekelezaji wa mfumo wa fedha.

1.3 Majukumu kuhusu taratibu zilizomo kwenye mwongozo

Makatibu Wakuu wa Wizara ya Elimu na Utamaduni (MoEC), na ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Ofisi ya Rais TAMISEMI), Sekretariati za mikoa (RS), na Wakurugenzi wa Halmashauri (CDs) wana wajibu wa kuhakikisha kuwa masharti yaliyowekwa katika mwongozo huu yanafuatwa na kutumiwa ipasavyo wakati wa utekelezaji wa programu hii.

Mhasibu Mkuu wa Serikali (ACCGEN) kama msimamizi mkuu wa mifumo ya hesabu ya serikali atawajibika kuhakikisha kwamba wakati wa utekelezaji wa masharti ya Mwongozo, masharti ya IMFS nayo yanatimizwa.

Wafanyakazi wanaohusika katika MoEC, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, RAS, Halmashauri za wilaya na shule watahakikisha kwamba shughuli za kila siku zinafuata taratibu zilizomo kwenye mwongozo huu.

MWONGOZO WA MEMM WA HESABU NA USIMAMIZI WA FEDHA

Ofisi ya Mdhidhibi na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG) na wakaguzi wa ndani waliopo kwenye ofisi za mikoa na wale wanaohudumia Halmashauri wana jukumu la kutathimini na kuhakikisha kwamba taratibu za fedha na vidhibiti zinafuata ipasavyo.

Wahasibu Wakuu wa MoEC, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, RS na **Watunza Hazina** wa Halmashauri watafuatilia kutimizwa kwa taratibu zilizowekwa katika Mwongozo huu.

1.4 Hatua za kinidhamu

Taratibu za hatua za kinidhamu kwa matumizi mabaya ya fedha za MMEM zitachukuliwa kwa mujibu wa taratibu za serikali na sheria nyingine husika.

2. MUUNDO WA KITAASISI NA MAJUKUMU

Uanachama wa kamati zote ni kama ulivyoielezwa katika kiambatisho cha Mpangilio wa kitaasisi kwa MMEM

2.1 Kamati ya Uendeshaji ya ESDP

Elimu ina jukumu la kuhakikisha kwamba unakuwepo mkabala wa sekta pana na ulioratibiwa na programu. Kamati itashughulikia masuala ya sera, kuratibu masuala baina ya Wizara na Wizara na kuhakikisha uwiano wa programu na sera nyingine za serikali. Katibu Mkuu katika ofisi ya Waziri Mkuu ndiye mwenyekiti wa kamati. Wajumbe wake wanatoka katika sekta za Wizara zinazohusika.

Wajibu wa kamati kuwa ni

- Kusimamia utekelezaji, maendeleo na utimizaji wa maamuzi ya Sera za Elimu ya Taifa.
- Kufuatilia MMEM
- Kufanya uratibu wa hall ya juu baina ya wizara na wizara.
- Kuhakikisha kwamba MMEM inafuata sera pana za serikali.

2.2 Kamati ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi (BEDC)

Kamati ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi ina jukumu la kusimamia maendeleo ya Elimu ya awali, ya msingi, sekondari, ualimu, elimu ya watu wazima na kuhakikisha kwamba inakamilisha malengo ya programu ya maendeleo ya sekta pana. Ndani ya muundo wa elimu ya msingi, BEDC ina lengo mahususi la kuongoza na kusimamia maendeleo katika elimu ya shule za msingi. Kamati hii ipo chini ya uenyekiti – wenza wa makatibu Wakuu wa MOEC na Ofisi ya Rais-TAMISEMI.

Wajumbe ni pamoja na Naibu Katibu Mkuu wa MoF, waratibu wa ESDP, MoEC na PO-RALG, wawakilishi 3 au 4 wa Asasi zisizo za kiserikali, Mkurugenzi wa Huduma za Menejiment Ofisi ya Rais-

MWONGOZO WA MEMM WA HESABU NA USIMAMIZI WA FEDHA

Utumishi, wawakilishi toka Wizara zinazohusika na Sekta ya Elimu, Wakurugenzi na Wakurugenzi wsaidizi wote wa MoEC na wahisani wanaochangia Sekta ya Elimu.

Majukumu ya BEDC kwa mujibu wa Usimamizi wa Fedha na Hesabu kwa MMEM ni:

- a) Kushirikiana na vyombo vya fedha na wadau wengine katika kutayarisha na kugharimia shughuli ziliopangwa;
- b) Kuwezesha kupatikana kwa rasilimali za kiufundi na kifedha ili kusaidia utekelezaji wa MMEM;
- c) Kukusanya rasilimali za serikari na za wahisani kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Elimu (EDF) ulioanzishwa kwa ajili hiyo kama sehemu ya Akaunti ya Jumla ya Hazina katika Benki Kuu ya Tanzania;
- d) Kuidhinisha Mpango wa Utekelezaji na Bajeti na utabiri wa mapato halisi ya robo mwaka;
- e) Kuanzisha na kupitia mara kwa mara taratibu za mipango za MMEM, usimamizi, ufuatiliaji na tathmini na ugharimaji.
- f) Kuidhinisha na kujadili ripoti za ukaguzi wa mahesabu na ripoti za fedha na kuchukua hatua za ufuatiliaji zinazofaa.
- g) Kuidhinisha utoaji wa fedha kutoka katika Akaunti ya pamoja.

2.3 Benki Kuu ya Tanzania

Majukumu ya Benki Kuu ya Tanzania kwa mujibu wa fungu la MMEM ni:

- a) Kuendesha Akaunti ya pamoja ya MMEM kama ilivyoelekezwa na BEDC; na
- b) Kutoa ripoti za ukaguzi wa mahesabu za kila robo ya mwaka katika akaunti ya pamoja.

2.4 Mhasibu Mkuu wa Serikali

Mhasibu Mkuu wa Serikali (ACCGEN) ana jukumu la:

- a) Kuhakikisha kwamba mifumo ya usimamizi wa fedha kwenye Wizara inasimamiwa vizuri.
- b) Uendeshaji wa Akaunti ya pamoja ya MMEM ikiwa ni pamoja na utunzaji wa kumbukumbu zilizo sawa za akaunti hiyo.
- c) Kufanya malinganisho ya hesabu za benki kila mwezi ya akaunti ya pamoja na kutoa taarifa yake kwenye BEDC kila baada ya robo mwaka.
- d) Kutoa taarifa za masuala ya matumizi ya fedha kwa vitengo vinavyotumia; na
- e) Kuiamuru BoT kulipa fedha kwenye akaunti za benki za Halmashauri na Wizara kama zilivyoidhinishwa na BEDC.

MWONGOZO WA MEMM WA HESABU NA USIMAMIZI WA FEDHA

2.5 Ofisi ya Rais–Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)

TAMISEMI ina jukumu la usimamizi wote wa Halmashauri na shule na itatekeleza yafuatayo;

- a) Katibu Mkuu, TAMISEMI atakuwa mwenyekiti mwenza wa BEDC
- b) Kwa kushirikiana na MoEC kusimamia matayarisho ya mipango ya maendeleo ya mwaka, bajeti na taarifa za vipindi kuhusu matumizi ya fedha za programu.
- c) Kusimamia Halmashauri kwa masuala yanayohusu utekelezaji wa programu.
- d) Kuhakikisha kwamba Halmashauri zote na RS zinawasilisha taarifa zao za vipindi kwa wakati.
- e) Kutayarisha ripoti fupi kwa Halmashauri zote na kuikabidhi kwa BEDC pamoja na mapendekezo.
- f) Kwa kushirikiana na MoEC, kuhakikisha kwamba taarifa za BEDC zinatayarishwa na kuwasilishwa kwa wakati.
- g) Kuchambua taarifa zote ili kuhakikisha kwamba Halmashauri na shule zinakidhi viwango vya chini vya kitaifa na viashiria vya utendaji vilivyowekwa.
- h) Kutayarisha maombi kwa ACCGEN kutoa taarifa za masuala ya matumizi ya fedha.
- i) Kuhakikisha kwamba vipengele vyote vya programu vinatekelezwa katika ngazi ya wizara pamoja na kujenga uwezo na uwezesaji unafanyika kwa uangalifu.
- j) Kutayarisha miongozo ya kitaifa kwa ajili ya matumizi ya shule na mgao wa fedha za MMEM.

2.6 Wizara ya Elimu na Utamaduni (MoEC)

MoEC ina jukumu la sera, ushauri wa kiufundi na ufuatiliaji wa masuala yanayohusu shule. Wajibu mahususi zaidi unajumuisha:

- a) Katibu Mkuu, MoEC ni mwenyekiti – Mwenza wa BEDC
- b) Wajibu wa kuendeleza na kufuatilia masuala yanayohusu miongozo ya elimu ya taifa, viashiria vya utendaji na viwango.
- c) Kutayarisha miundo kwa ajili ya taarifa ya elimu ya ufundi ya Halmashauri.
- d) Kupitia mipango ya Sekta ya Elimu ya Halmashauri ili kuhakikisha kuwa masharti ya sera na miongozo ya sekta ya kitaifa yanayotimizwa
- e) Kuishauri Ofisi ya Rais-TAMISEMI kuhusu utendaji wa kiufundi wa Halmashauri.
- f) Kurekebisha huduma za sekta ya elimu nchini.
- g) Kusaidia Sekretariati za Mikoa kuhusu masuala ya kiufundi.
- h) Kuhakikisha kwamba taarifa kwa ajili ya sehemu inazozishughulikia zinatayarishwa na kuwasilishwa kwa wakati katika BEDC.

MWONGOZO WA MEMM WA HESABU NA USIMAMIZI WA FEDHA

- i) Kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI, kushauri kuhusu matayarisho ya mipango ya maendeleo ya mwaka, bajeti na taarifa za vipindi kuhusu matumizi ya mfuko wa fedha wa pamoja.
- j) Kuhakikisha kwamba mambo yote yanayohusu utekelezaji wa programu katika ngazi ya Wizara ikiwemo kujenga uwezo wa wafanyakazi na uwezesaji unafanyika
- k) Kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI kupendekeza kwa IMSC na/au BEDC kuhusu utoaji wa fedha kwa Halmashauri na shule.
- l) Kubuni mbinu za ufuatiliaji na upimaji wa utendaji wa huduma za sekta ya elimu na Halmashauri.
- m) Kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI, kuhakikisha kwamba taarifa kwa ajili ya BEDC zinatayarishwa na kuwakilishwa kwa wakati.
- n) Kutayarisha maombi kwa ajili ya ACCGEN, kutoa taarifa za masuala ya Mautmizi ya Fedha na kuhamishia mafungu ya fedha kwa MoEC.

2.7 Sekretariati ya Mkoa

Sekretariati ya mkoa ni tawi la Ofisi ya Rais-TAMISEMI mikoani. Ina wataalamu wa kusaidia huduma katika sekta za jamii, sekta za mipango na uhandisi, sekta ya maendeleo ya uchumi na sekta ya usimamizi. Haina budi kuisaidia Ofisi ya Rais-TAMISEMI katika utekelezaji wa kazi zake katika Halmashauri. Aidha, itatekeleza wajibu ufuatao:

- a) Kuunga mkono na kusaidia Halmashauri katika matayarisho ya mipango ya maendeleo na mipango ya utekelezaji.
- b) Kuishauri Halmashauri kuhusu masuala yanayohusu matayarisho ya taarifa za vipindi/utendaji.
- c) Kuhakiki ripoti kwa ajili ya kupatana na sera za taifa na miongozo, usahihi wa namba, usahihi wa bakaa ya kufungulia na kufungia, mafungu yanayoonekana kuwa si ya kweli kutokana na ukubwa na ufuatiliaji katika Halmashauri au wizara kadri inavyoonekana inafaa.
- d) Sekretariati za mkoa zitasaidia mamlaka za ukaguzi wa mahesabu wa ndani kupitia katika shughuli za ukaguzi wa ndani.

2.8 Halmashauri

Halmashauri ina jukumu la:

- a) Kusimamia matayarisho ya mipango ya shule na bajeti.
- b) Kuzisaidia shule kuhusu utunzaji bora wa fedha wanazopewa ikiwa ni pamoja na kufungua na kuendesha akaunti za benki.
- c) Kuhamishia fedha katika akaunti ya benki ya shule kwa wakati muafaka.
- d) Kuhakikisha kwamba fedha zinazolipwa shule zinatumiwa kufuatana na miongozo ya taifa kwa MMEM.

MWONGOZO WA MEMM WA HESABU NA USIMAMIZI WA FEDHA

- e) Kuhakikisha kwamba taarifa za shule zinatayarishwa na kuwasilishwa kwa wakati.
- f) Kutayarisha taarifa za vipindi/utendaji kwa ajili ya Halmashauri, ambayo ni mkusanyiko wa taarifa za shule.
- g) Kupeleka kwa wakati vitabu na vifaa vingine vya kujifunzia.
- h) Ukaguzi wa ndani wa uendeshaji shule
- i) Kuhamasisha kamati za shule
- j) Kutayarisha mpango wake kwa ujenzi wa uwezo na uwezesaji wa shughuli za shule.
- k) Kuhakikisha kwamba kanuni na taratibu za serikali zinafuatwa ipasavyo wakati wa kutekeleza programu za Halmashauri.
- l) Kuhakikisha kwamba taarifa zote za robo mwaka na za mwaka (fedha na utendaji) zinawasilishwa mbele ya madiwani wakati wapokutana.


2.9 Kamati ya shule

Kama ya shule ina majukumu yafuatayo;

- a) Kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mtaa/kijiji, itatayarisha na kurekebisha mipango ya maendeleo ya shule na mipango ya utekelezaji.
- b) Kuhakikisha utunzaji mzuri wa fedha inazopewa, ikiwa ni pamoja na kufungua akaunti ya benki ya shule na kuiendesha kwa mujibu wa taratibu zilizotolewa na Halmashauri.
- c) Kuhakikisha kwamba shughuli zilizothibitishwa na BEDC zinatekelezwa kama zilivyopangwa.
- d) Kutayarisha taarifa kama itakavyoelekezwa na Ofisa Elimu wa Halmashauri (Mratibu wa Programu) katika ngazi ya Halmashauri.
- e) Kuwasilisha kwa Halmashauri hati zote zinazohusiana na utekelezaji wa programu kwa madhumuni ya kuelezea matumizi na hesabu.

MWONGOZO WA MEMM WA HESABU NA USIMAMIZI WA FEDHA

Kielelezo 1: MUUNDO WA UTAWALA WA ESDP NA UENDESHAJI WA MASUALA YA FEDHA



Programu ya kutekeleza masuala ya fedha hutetelezwa kwa mujibu wa muundo ulipo wa fedha za serikali. Maafisa fedha wanaohusika katika wizara, Halmashauri na shule watakuwa wahusika wakuu wa masuala ya fedha za programu.

3. MIPANGO NA BAJETI

3.1 Mipango katika MoEC na Ofisi ya Rais-TAMISEMI

Mipango ya shughuli za MEMM kwa Ofisi ya Rais-TAMISEMI /MoEC itafuata mchakato wa mipango ya kawaida ya Serikali ya Tanzania, pamoja na shughuli za MEMM zilizojumuishwa katika mpango mzima wa taifa kufuatia makubaliano ya IMSC. Mipango ya kila mwaka inayotokana na mipango ya taifa itaunda msingi wa matayarisho ya bajeti ambayo pia yatafuata taratibu za kawaida za Serikali na bajeti kwa ajili ya shughuli za MEMM. Aidha, itajumuishwa katika bajeti ya Wizara itakayopitishwa na Bunge.

3.2 Mipango katika ngazi ya Halmashauri

Mipango inaandaliwa katika sekta nzima kwa mapana katika ngazi ya Halmashauri na kutayarishwa kulingana na taratibu za Ofisi ya Rais-TAMISEMI za mipango ya ushirikishwaji. Aidha zitaundwa kutoka katika ngazi ya shule na kuunganishwa katika Mipango ya Elimu ya Halmashauri.

MWONGOZO WA MEMM WA HESABU NA USIMAMIZI WA FEDHA

Katika sehemu hii tutaeleza kwa muhtasari matokeo ya mchakato wa mipango ambayo yanaunda msingi wa matayarisho ya bajeti na muundo wa bajeti na maudhui. Mchakato yenyewe imeelezwa katika Mwongozo wa mipango ya Ushirikishwaji wa serikali za mitaa.

Matokeo ya mchakato wa mipango ya Halmashauri na ngazi zilizoidhinishwa ni:

Hati	Imetayarishwa na	Imeidhinishwa na	Imechunguzwa na
Mpango wa shule wa miaka 3	Kamati ya shule	<ul style="list-style-type: none"> Halmashauri ya mtaa/kijiji Halmashauri 	
Mpango wa Elimu wa miaka 3 wa Halmashauri	Halmashauri	Halmashauri	<ul style="list-style-type: none"> Mkoa Ofisi ya Rais-TAMISEMI /MoEC
Mpango wa shule wa utekelezaji na Bajeti (POAB)	Kamati ya shule	<ul style="list-style-type: none"> Halmashauri ya mtaa/kijiji Halmashauri 	
Mpango wa elimu wa mwaka wa Halmashauri	Halmashauri	<ul style="list-style-type: none"> Halmashauri 	<ul style="list-style-type: none"> Mkoa Ofisi ya Rais-TAMISEMI /MoEC

Mpango wa Halmashauri wa miaka mitatu umejikita katika mpango wa shule wa miaka 3 na mpango wa mwaka wa elimu na Mipango ya shule na utekelezaji wa Bajeti inatayarishwa ndani ya muundo wa mpango wa miaka 3.

3.2.1 Mpango wa utekelezaji na Bajeti wa shule kwa mwaka.

Kila shule itatayarisha mpango wa miaka 3 ambao utawasilishwa kwa halmashauri kwa ajili ya kuidhinishwa. Mpango huu utatoa muundo kwa ajili ya matayarisho ya Mpango wa shule na utekelezaji wa Bajeti.

3.2.2 Mpango wa Elimu wa Halmashauri

Mipango ya utekelezaji na Bajeti ya Shule (PoAB's) itathibitishwa na Halmashauri na kuunganishwa katika Mpango wa Elimu wa Halmashauri kwa pamoja na mipango ya sekta nyingine katika ngazi ya Halmashauri. Hii itakuwa katika muundo mmoja na muhtasari hapo juu.

3.3 Kufanya bajeti kwa Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa ajili ya matumizi ya mfuko wa Fedha wa Programu ya Elimu.

Ili kutoa huduma zilizokusudiwa katika MEMM, itakuwa ni muhimu kwa Wizara ya Elimu na Utamaduni kutambua na kugharimia mikakati/shughuli katika misingi ya pembejeo zinazotakiwa

MWONGOZO WA MEMM WA HESABU NA USIMAMIZI WA FEDHA

kufikiwa/kupokea huduma hizo. Baadhi ya pembejeo zitajirudia kila mwaka, na inapaswa ziainishwe kama matumizi yanayojirudia.

Hatua zitakazofuatwa zitakuwa ni zile zinazotumika katika utayarishaji wa Bajeti ya serikali. Hata hivyo, hapa chini tumetoa hatua mahususi zinazotakiwa katika kuingiza matumizi ya MMEM katika bajeti.

3.3.1 Kutoa fedha za Bajeti

Bajeti za Wizara ya Elimu na Utamaduni na Ofisi ya Rais-TAMISEMI, MMEM zinagharimiwa

- a) Kutoka katika mapato ya ndani yanayokusanywa na serikali ya Tanzania.
- b) Kutoka katika ahadi za ruzuku na mikopo kutoka kwa wahisani wabia katika mfuko wa fedha wa MMEM
- c) Kupitia mfuko wa fedha utakaopokelewa toka katika mfuko wa pamoja kama msaada wa bajeti

3.3.2 Taratibu za kufuatwa wakati wa kuandika bajeti ya matumizi yanayojirudia ni kama zifuatazo:

Bajeti ya kawaida inajumuisha mapendekezo kwa ajili ya ununuzi wa vitabu vya shule, matengenezo madogo ya vifaa na uendelezaji wa stadi za utaalumu.

- a) SC kupitia upya malengo ya muda mrefu yaliyowekwa na Wizara ya Elimu na Utamaduni na kuhakikisha kwamba shughuli zinafanywa kwa mujibu wa matakwa ya MMEM.
- b) Ofisi ya Rais-TAMISEMI na Wizara ya Elimu na Utamaduni kuorodhesha shughuli za Wizara ya Elimu na Utamaduni na shughuli zitakazofanywa na Halmashauri. Hii itajumuisha kupitia mikakati ya kila wizara ili kuainisha malengo, shughuli na rasilimali zinazohitajika (pembejeo).
- c) Ofisi ya Rais-TAMISEMI na Wizara ya Elimu na Utamaduni kupima pembejeo kwa kila shughuli kwa makubaliano ya kifedha (gharama)
- d) MoEC kubainisha matokeo kwa kuzingatia shughuli. Kwa mfano, idadi ya watumishi waliopata mafunzo katika mpango wa mradi wa elimu na msaada wa usimamizi wa kiufundi uliotolewa.
- e) Ofisi ya Rais-TAMISEMI na Wizara ya Elimu na Utamaduni kupitia makisio yaliyotayarishwa ili kuhakikisha kwamba hayazidi matumizi ya juu na yanakubaliana na vipaumbele vilivyowekwa; na
- f) Wizara ya Elimu na Utamaduni kuweka vigezo vya ufanisi wa shughuli kwa mfano; uwiano wa gharama za shughuli utakaotumika. Huu ni uwiano wa rasilimali zilizopangwa katika shughuli kwa kiasi cha matokeo ya shughuli husika.

MWONGOZO WA MEMM WA HESABU NA USIMAMIZI WA FEDHA

BEDC itapitia sehemu muhimu za mfumo wa matumizi ya muda wa kati kabla ya kuwasilisha kwa Wizara ya Fedha, ikitoa maoni kupitia Wizara ya Elimu na Utamaduni na Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa kuzingatia makisio ya matumizi ya mfuko wa fedha wa MMEM.

3.3.3 Bajeti ya matumizi ya maendeleo

Bajeti ya maendeleo inajumuisha mapendekezo kwa matumizi katika maendeleo ya miradi kama vile ujenzi na ukarabati wa madarasa, nyumba za walimu, na vifaa vya udhibiti wa afya. Idara ya Sera na Mipango inawajibika kutayarisha bajeti za matumizi ya maendeleo.

Miradi yote inayojumuishwa katika bajeti ya matumizi ya maendeleo haina budi kusaidiwa na yafuatayo;

- a) Anwani inayojeleza vizuri
- b) Gharama ya kifaa, ikiwa pamoja na gharama za kawaida kama matengenezo na ukarabati., gharama za kawaida kama hizo hazina budi kujumuishwa katika gharama za bajeti ya kawaida;
- c) Mapendekezo ya awali na tarehe ya kuisha
- d) Faida zinazoendana na mradi kwa kuzingatia mafanikio ya malengo ya sekta ya elimu na mafanikio ya mpango wa muda mrefu wa Wizara ya Elimu na Utamadun

Mara bajeti ya maendeleo ya mwaka itakapokuwa imetayarishwa na Idara ya Sera na Mipango itakabidhiwa kwa BEDC kwa ajili ya kupitiwa na kuidhinishwa na baada ya hapo inapitia katika mfumo wa bajeti wa Serikali. Bajeti iliyoidhinishwa inapelekwa kwa Kamishna wa Bajeti kwa ajili ya kuingizwa IFMS.

Matumizi kwa ajili ya mwaka wa kwanza wa uendeshaji wa MMEM yatapangiwa bajeti na fedha zitapitishwa katika bajeti ya maendeleo. Baada ya hapo, inatarajiwa kwamba MMEM itaungana kabisa na bajeti ya kawaida.

3.4 Bajeti katika Ngazi ya Halmashauri kwa ajili ya Mfuko wa Programu ya Elimu

3.4.1 Vyanzo vya mapato

Vyanzo vya mapato kwa ajili ya Programu za elimu katika ngazi ya Halmashauri ni:

- a) Misaada ya masharti kutoka Serikali Kuu
- b) Mapato ya kodi ya ndani
- c) Fedha za msaada kutoka mfuko wa MMEM (bila kujali chanzo cha fedha)
- d) Jumuiya ya shule
- e) Programu sambamba na wahisani
- f) Asasi zisizo za kiserikali (AZISE)

MWONGOZO WA MEMM WA HESABU NA USIMAMIZI WA FEDHA

3.4.2 Ruzuku kutoka katika mfuko wa MEMM

Shule za msingi zitapata ruzuku kutoka katika mfuko wa ESDP. Ruzuku hiyo itafidia gharama za uendeshaji zinazoongezeka pamoja na gharama za maendeleo kama zilivyofafanuliwa hapa chini.

Ruzuku itagawanywa katika:

- i. Ruzuku maalum kwa kila mwanafunzi
- ii. Ruzuku ya maendeleo

Shule za msingi zitapokea fedha za ruzuku ya maendeleo na fedha za ruzuku kwa kila mwanafunzi.

3.4.3 Ruzuku maalumu kwa kila mwanafunzi

Programu itazipa shule zote za msingi ruzuku maalumu kwa kila mwanafunzi. Kiasi cha fedha kitategemea idadi ya wanafunzi walioandikishwa shule. Uandikishaji kwa madhumuni ya kutayarisha bajeti utategemea wastani wa uandikishaji wa miaka iliyopita na kurekebisha kwa mujibu wa mabadiliko yanayotarajiwa. Utaratibu utakaotumika kupanga bajeti ya ruzuku maalumu kwa kila mwanafunzi kwa ajili ya shule itapatikana kwa utaratibu ufuatao:

- Idadi ya wanafunzi wanaohudhuria itakadiriwa katika kupanga bajeti kwa kuangalia wastani wa mahudhurio kwa mwezi Machi na Septemba wa mwaka wa kuamaliza masomo.
- Kwa wale watakaokuwa darasa la 2 hadi la 7 mwaka 2002, idadi ya uandikishaji itajulikana kwa kuchukua wastani wa uandikishaji wa darasa la 1 hadi la sita mwezi Machi na Septemba 2001. Idadi hii haitarajiwi kubadilika kwa mwaka 2002 (mwaka wa 1 tu).
- Kwa wale watakaokuwa darasa la 1 mwaka 2002 idadi ya uandikishaji itajulikana kwa kuchukua wastani wa uandikishaji itajulikana kwa kuchukua wastani wa uandikishaji wa darasa la 1 mwezi Machi na Septemba 2001 na kurekebisha kwa kiwango cha 1.8 (mwaka wa 1 tu).

BEDC itapitia upya na kurekebisha kiasi hicho kila mwaka kutegemea mfumko wa bei na sababu nyingine.

Ruzuku maalum kwa kila mwanafunzi itagharamia matumizi ya mafungu yaliyoelezwa katika bajeti ya matumizi ya kawaida na kujumuisha vifaa kama vile vitabu vielelezo vya kufuadishia, vifaa vya matumizi ya kila siku, gharama za michezo, n.k. Fedha hizo pia zitagharamia matumizi ya ukuzaji wa stadi za kitaalamu zisizokuwa za mafunzo endelevu. Kamati ya shule itakuwa na jukumu la kuhakikisha kwamba msaada unaotolewa unapangwa ipasavyo katika mafungu ya bajeti kwa kusudi la kutimiza malengo ya mpango wa shule.

MWONGOZO WA MEMM WA HESABU NA USIMAMIZI WA FEDHA

Matumizi ya msaada wa utoaji taarifa ya mahitaji ni kama ilivyoanishwa katika vifungu vinavyohusu matumizi ya fedha na utoaji taarifa.

3.4.4 Ruzuku ya Maendeleo

Shule za msingi zitapokea fedha za ruzuku ya maendeleo kwa ajili ya samani na vifaa (viti, madawati, meza, n.k), ujenzi wa majengo (majengo mapya au ukarabati wa madarasa na nyumba za walimu)

Ruzuku hii italipwa shuleni kwa msingi wa bajeti ya maendeleo (uwekezaji) iliyotayarishwa sambamba na mpango wa utekelezaji wa shule na kuthibitishwa na Halmashauri.

Utaratibu utakaotumika kuthibitisha matumizi na kutoa fedha za ruzuku na maendeleo na kikao cha BEDC ni ule ule unaotumika kwa fedha za ruzuku kwa kila mwanafunzi.

Katika muda wote wa programu hii, shule zote zitapokea ruzuku ya fedha za maendeleo, hata hivyo baadhi ya shule zinaweza zisipokee fedha za ruzuku ya maendeleo. Fedha za ruzuku ya maendeleo zitatolewa tu kwenye shule zitakazokuwa zinatoa taarifa sahihi za robo mwaka mpango mzima na mpango wa nyinyi uliothibitishwa na Halmashauri.

Ruzuku itatolewa kwa msingi wa robo mwaka kutegemea kupatikana kwa taarifa za utekelezaji za robo mwaka kama ilivyoelezwa katika kifungu cha matumizi. Taarifa zitaambatanishwa na kuthibitishwa na Mhandisi wa Halmashauri au mtu binafsi aliyeteuliwa kwa ajili hiyo akithibitisha kiwango cha ukamilishaji wa ujenzi, ambazo pia zitaonyesha iwapo viwango vya ujenzi vilivyoelekezwa na maelekezo yaliyotolewa na Wizara ya Elimu na Utamaduni vimefuatwa.

3.4.5 Utayarishaji wa Bajeti

Shule zitatarisha bajeti za kawaida na maendeleo katika POABs. Bajeti zitawasilishwa katika muundo uliotolewa katika kiambatisho B na kupitishwa na Halmashauri ili zijumuishwe katika mpango wa Bajeti ya Elimu ya Halmashauri. Halmashauri itaitaarifu shule kuhusu kiasi cha bajeti kilichopitishwa na Halmashauri wakati wa kukamilisha bajeti ya Halmashauri.

Bajeti ya shule inajumuisha mapato yote na matumizi ambayo yanategemea kupitia katika akaunti ya shule na kupanga mapato dhidi ya vyanzo mbalimbali vya fedha.

Bajeti ya Elimu ya Halmashauri inapitia katika sekretariati ya Mkoa kwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI ambao watawasilisha kwa BEDC kwa kupitisha kiwango cha fedha kitakachotolewa katika programu.

MWONGOZO WA MEMM WA HESABU NA USIMAMIZI WA FEDHA

3.5 Ratiba ya upangaji na bajeti

Na.	Shughuli	Mchukua Hatua	Muda
1.	Taarifa kuhusu mchakato na upangaji inatolewa kwa ngazi zote za shule na Halmashauri	Mratibu wa Programu ya MEMM (MoEC na Ofisi ya Rais -TAMISEMI	Machi-Mei
2	Matayarisho ya Mpango wa elimu wa Halmashauri na Bajeti	Halmashauri/kamati za shule	Julai
3	Mpango wa elimu na Halmashauri kujadiliana katika ngazi ya Halmashauri/Mji/Wilaya/Jiji	Mkurugenzi/Jiji/mj/Halmashauri/Wilaya	Septemba
4.	Bajeti ya elimu ya Halmashauri kujadiliwa katika ngazi ya Mkoa	RAS	Septemba
5.	Halmashauri kutayarisha bajeti kulingana	Mkurugenzi wa Halmashauri na menejimenti	Oktoba
6	Bajeti kujadiliwa katika ngazi ya mkoa	RS	Oktoba
7	Bajeti za Halmashauri kujadiliana na Halmashauri	Mkurugenzi Halmashauri	Novemba
8	Bajeti za Halmashauri kujadiliwa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI	Mratibu wa programu MEMM Ofisi ya Rais-TAMISEMI	Mwanzoni mwa Desemba
9	Mipango/utekezaji wa Bajeti kuwasilisha BEDC	Mratibu program MEMM-MoEC na Ofisi ya Rais-TAMISEMI	Mwishoni wa Desemba

4. ULIPAJI FEDHA

4.1 Uendeshaji wa Akaunti ya pamoja ya MEMM

4.1.1 Uhamishaji fedha katika Akaunti ya pamoja ya MEMM

Fedha za MEMM zinapatikana kutoka Serikali ya Tanzania, kikundi cha wahisani kinachochangia ama kwa kiupitia Mfuko wa fedha wa Pmoja au moja kwa moja Hazina na jumuiya za maeneo.

Kufuata muundo na mwongozo wa usimamizi wa feha inatarajiwa kuwa wachangiaji wa mpango watatoa fedha mapema kwa msingi wa Mipango ya utekezaji ya Halmashauri/shule. BEDC itakuwa na jukumu la kuainisha kwa msingi wa kila mwaka mahitaji yatakayoongoza wabia kuhusu kiasi cha fedha kitakachohamishiwa hazina moja kwa moja au kupitia Akaunti ya fedha ya pamoja.

Kiasi cha fedha kitakachohamishwa moja kwa moja kwenye Akaunti ya fedha ya pamoja kitawekwa mipaka ili kuhakikisha kwamba kinatumika kwa madhumuni ya elimu tu. Vilevile, fedha zitakazotolewa kupitia katika akaunti hiyo zitawekwa na matumizi yake kuelezwa katika akaunti ya **zuio** iliyopo Benki Kuu ya Tanzania.

MWONGOZO WA MEMM WA HESABU NA USIMAMIZI WA FEDHA

Akaunti ya pamoja ya MEMM itawekwa katika Benki Kuu ya Tanzania (BoT). BoT ina jukumu la kutoa Akaunti za Benki za serikali. Wahisani wabia wataweka fedha za kigeni BoT katika Akaunti ya pamoja ya MEMM, fedha ambazo ni za kugharimia mipango na bajeti za sekta ya elimu.

Ama Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu na Utamaduni au Ofisi ya Rais-TAMISEMI, kwa idhini ya BEDC watakuwa na mamlaka ya kumuelekeza Mhasibu Mkuu kuomba kulipwa kutoka katika akaunti kwa ajili ya shughuli ambazo kila wizara inahusika kipekee.

Idara ya Mhasibu Mkuu, vitengo vya mapato na Hazina vitawajibika na usimamiaji wa akaunti, ikiwa ni pamoja na malinganisho ya benki kila mwezi na utoaji wa ushauri wa miamana ya Benki kwa fedha zilizozingizwa katika akaunti. Watia saina katika akaunti hii watakuwa mtu mmoja kutoka katika kila makundi yafuatayo

Kundi A Mhasibu Mkuu
Msaidizi wa Mhasibu Mkuu

Kundi B Wahasibu wakuu wawili kutoka ofisi ya ACCGEN

Watatoa idhini ya kutoa fedha katika Akaunti ya pamoja ya MEMM kwa maelekezo kutoka kwa Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu na Utamaduni/ Ofisi ya Rais-TAMISEMI yakiambatana na nakala ya kumbukumbu za mkutano wa kamati ya mfuko wa fedha.

Utaratibu ufuatao utatumika katika kutoa fedha katika Akaunti ya pamoja ya MEMM;

- Kila robo mwaka Maofisa wahasibu (Wizara ya Elimu na Utamaduni na Ofisi ya Rais-TAMISEMI) kwa kushirikiana na Mkurugenzi wa Sera na Mipango (DPP) katika wizara watatayarisha mpango wa robo mwaka ambao uaneleza shughuli na mambo yatakayotimizwa katika kipindi cha robo mwaka pamoja na mahitaji ya fedha kufuatana na bajeti ya wahisani wabia na serikali ya Tanzania.
- Ofisa Mhasibu kwa kushirikiana na Mkurugenzi wa Sera na Mipango na wadhamini watatayarisha makisio ya mapato halisi (kiambatisho 2D) yakizingatia mpango wa utekezaji iliyothibitishwa. Makisio ya mapato halisi yataonyesha mahitaji yanayohitaji fedha kwa kipindi cha robo mwaka kwa vyanzo vya fedha kutoka serikali ya Tanzania, MEMM na vyanzo vingine.
- Katika kutayarisha makisio ya mapato halisi, Mhasibu Mkuu kwa kushauriana na Mkurugenzi wa Sera na Mipango na **wadhamini** hawana budi kuzingatia: mapato halisi ya Halmashauri, mipango ya shughuli zitakazofanywa katika robo inayofuata ikizingatia shughuli za robo iliyoisha ambazo bado zinatekelezwa; vidokezo vya kifedha

MWONGOZO WA MEMM WA HESABU NA USIMAMIZI WA FEDHA

kwa kuangalia mapato halisi; na matarajio ya kuyapata hayo mapato halisi.

- Maofisa wa uhasibu watawasilisha mpango wa robo mwaka na mapato halisi yanayotarajiwa kwa BEDC kwa ajili ya kupitiwa na kuthibitishwa.
- Wahisani wabia katika mpango wa kuchangia watautumia mpango huu kutoa fedha Benki Kuu katika Akaunti ya pamoja ya MMEM.
- Benki Kuu ya Tanzania itatoa ushauri wa miamana ya Benki kwa Mhasibu Mkuu kumtaarifu kwamba benki imetoa mkopo katika Akaunti ya pamoja ya MMEM kwa fedha zilizopokelewa kutoka kwa wahisani wabia. Ofisa Mhasibu atatumia jalada la mikopo yote ya benki iliyoshauriwa katika akaunti hii. Kwa madhumuni ya mahitaji ya mhisani mbia kupitia mahesabu binafsi, nakala zitatumwa kwa wahisani wabia zitakapokelewa.
- Katika kupokea miamana ya Benki, Mhasibu Mkuu anatoa stakabadhi ya vocha katika nakala tatu. Nakala ya kwanza itapelekwa kwa mhisani mbia, nakala zitahifadhiwa pamoja na hati zake (miamana na hati za Benki) na zitahifadhiwa kama kitabu cha nakala. Waendeshaji wa IFMs katika ofisi ya Mhasibu Mkuu watumia nakala ya satakabadhi ya vocha kutengeneza upya daftari ya fedha katika IFMs.

4.1.2 Kupeleka fedha katika Akaunti ya mapato ya maendeleo

Fedha zinazopokelewa katika Akaunti ya pamoja ya MMEM zitatolewa kila baada ya robo mwaka katika akaunti ya Wizara ya Fedha inayotunzwa na Hazina. Taratibu zifuatazo zitatumika katika kutoa fedha katika Akaunti ya pamoja ya MMEM;

- Mhasibu Mkuu atawasilisha makisio ya mapato halisi kwa robo mwaka inayofuata na ripoti ya utendaji (kifedha na kiufundi) kwa ajili ya robo ya pili kutoka mwisho, atawasilisha kwa BEDC kwa ajili ya kuhakikiwa na kuthibitishwa,
- Makisio ya mapato halisi yaliyothibitishwa na ripoti inayoridhisha vitakuwa msingi kwa BEDC kuidhinisha utoaji wa fedha katika Akaunti ya pamoja ya MMEM,
- Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu na Utamadun au Ofisi ya Rais-TAMISEMI watamjulisha kwa maandishi Mhasibu Mkuu aielekeze Benki Kuu kuhamisha fedha kutoka katika Akaunti ya pamoja ya MMEM kwenda katika Akaunti ya Maendeleo ya Mapato. Wanapokea maelekezo ya kuhamisha, Benki Kuu watahamisha fedha katika Akaunti ya Wizara na kutoa miamala kwa msaada wa Mhasibu Mkuu.
- Ofisa Mhasibu atatoa taarifa ya kutolewa kwa akaunti ya Wizara ili kuziarifu pande zinazohusika (Wizara ya Elimu na Utamaduni na/au Ofisi ya Rais-TAMISEMI na Ofisi Kuu ya Malipo – CPO) kwamba fedha zipo. Matoleo katika Akaunti ya wizara lazima yaonyeshe chanzo cha fedha kama ni serikali ya Tanzania au fedha kutoka kwa wahisani wabia katika utaratibu wa MMEM. Ofisi Kuu ya

MWONGOZO WA MEMM WA HESABU NA USIMAMIZI WA FEDHA

Malipo itaingiza katika daftari ya fedha ya wizara husika katika Mfumo Mkuu wa malipo kiasi kilichohamishwa kutoka Akaunti ya mapato ya maendeleo.

- Ofisi Kuu ya Malipo katika Wizara ya Fedha itahamishia ruzuku moja kwa moja kwenye Akaunti Na. 5 ya halmashauri husika.

4.1.3 Taratibu za mwisho wa mwaka

Mwishoni mwa mwaka wa fedha baki isiyotumika katika makao makuu kutoka kwenye fedha za wahisani za MMEM zitahamishiwa kwenye Akauti ya Amana katika Wizara ya Fedha. Fedha hizi zitatumika sambamba na mafungu yatakayotolewa kwenye mwaka mpya wa fedha.

4.1.4 Taratibu za viwango vya ubadilishaji

Akaunti ya pamoja ya MMEM itaendeshwa katika fedha za kigeni lakini mafungu yatakayohamishwa kutoka kwenye akaunti hii kwenda kwenye akaunti ya Wizara kutafanywa katika shilingi. Hivyo pata- kuwepo na haja ya kubadilisha kiasi kilicho katika fedha za kigeni kuwa katika shilingi za Tanzania.

Ili kutambua kuongezeka au kupungua itakuwa muhimu kuweka kumbukumbu za viwango vya ubadilishaji vilivyotumika katika tarehe ya kuingiza fedha katika Akaunti ya pamoja ya MMEM na tarehe ya kufanya uhamisho wa fedha toka kwenye Akaunti ya pamoja.

Idara ya madeni ya serikali chini ya Mhasibu Mkuu itawajibika kwa utoaji wa kila siku wa viwango rasmi vya ubadilishaji kutoka BoT (viwango vya kuuza na kununua) katika IFMS kulingana na taratibu zilizopo. Kila patakapokuwepo miamala inayohusisha akaunti ya Pamoja ya MMEM, basi IFMS itachukua mara moja kiwango kinachofaa na kukokotoa kuongezeka au kupungua kunakosababishwa na mabadiliko ya viwango vya ubadilishaji kati ya muda wa kuingiza fedha hadi muda wa kuzihamishia kwenye akaunti ya Wizara. Kuongezeka au kupungua kutaripotiwa kwenye leja kuu na kuonyeshwa katika vyanzo na matumizi ya fedha.

4.2 Kupeleka kwenye Wizara/Idara

Baada ya kupokea Taarifa ya kutolewa kwa fedha za Wizara Ofisa Uhasibu atenga fedha hizo kwa wenye mafungu mbalimbali kwa kutoa Ripoti ya Taarifa ya Idhini ya Mafungu hadi kiwango cha juu kinachorudhisiwa kutolewa na Wizara. Ripoti hii itamuidhinisha kila mwenye Fungu kutumia fungu alilotengewa kwa ajili ya shughuli zilizoonyeshwa kwenye fungu.

Baada ya hapo taratibu zitafuata mfumo wa mahesabu wa kawaida wa Serikali.

MWONGOZO WA MEMM WA HESABU NA USIMAMIZI WA FEDHA

4.3 Kupeleka kwenye Halmashauri/shule

4.3.1 Kustahiki

Halmashauri zinapaswa kuripoti uendeshaji wa Akaunti No 5. Kila baada ya robo mwaka utoaji wa fedha na BEDC utaanza kwa halmashauri kupokea kutoka kila shule;

- Muhtasari wa maelezo ya matumizi halisi hadi tarehe hiyo na fedha zilizotolewa na MEMM na vyanzo vingine hadi tarehe hiyo kwa robo ya pili toka mwisho.
- Muhtari wa ripoti ya mipango na mafanikio halisi, na sababu za kuhitilafiana katika kipindi hicho cha robo mwaka ya pili toka mwisho.
- Muhtasari wa mpango wa utekelezaji kwa ajili ya robo mwaka inayofuata ikionyesha kiasi cha fedha kilichoombwa kwa kila shughuli.
- Katika robo ya kwanza tu, mpango wa utendaji na bajeti.
- Katika robo ya pili tu, hesabu ya mapato na matumizi kwa kipindi cha mwaka uliopita.

Taarifa za ukaguzi za halmashauri na wizara ni lazima ziwasilishwe ndani ya kipindi cha miezi sita baada ya mwisho wa mwaka wa fedha.

Shule zote zinastahiki kupata fedha za mpango. Shule zitategewa fedha kwa mfumo wa ruzuku. Ruzuku itagharimia shughuli za uendeshaji pamoja na shughuli za maendeleo. Ruzuku itagawanywa katika ruzuku ya matumizi ya kawaida (ruzuku wiani) na ruzuku ya maendeleo (ruzuku wekezi).

Kuweza kupata kiasi chote cha ruzuku ya matumizi ya kawaida na ruzuku ya maendeleo kutatawaliwa na kuwepo kwa mipango ya maendeleo inayojumuisha miaka mitatu na mpango wa utekelezaji kwa mwaka mmoja. Mipango itabidi iandaliwe kwa kuzingatia hali halisi ya mazingira ya shule na maelekezo mengine ya halmashauri. Katika mwaka wa 1, shule zitapokea kiasi kidogo cha ruzuku iwapo hazitakuwa na uwezo wa kuandaa mpango wa Maendeleo wa miaka mitatu au Mpango wa Utendaji na Bujeti.

Ofisi ya Rais-TAMISEMI ina wajibu wa kisheria wa kuhakikisha kwamba kila halmashauri inawasilisha mipango na bajeti bila kushindwa, vinginevyo shule hazitapatiwa fedha.

Ofisi ya Rais-TAMISEMI inapaswa kuhakikisha kuwa halmashauri zote zinazingatia ratiba ya kupanga mipango na kubajeti.

Ni kwa mwaka wa kwanza tu, sehemu ya vitabu katika ruzuku ya matumizi ya kawaida sawa na \$4 itatolewa kupitia kwenye halmashauri kwa kufikiria uwezo mdogo wa kununua vitabu uliopo katika ngazi ya shule. Halmashauri zitawajibika kwa ununuzi wa vitabu, lakini uchaguzi wa vitabu vya kiada vya kununua ni suala linaloihusu shule yenyewe.

MWONGOZO WA MEMM WA HESABU NA USIMAMIZI WA FEDHA

Ruzuku ya maendeleo kwa shule za msingi itatumika kugharimia ujenzi wa madarasa mapya na ukarabati mkubwa katika majengo yaliyopo. Ruzuku hii itategemea bajeti ya maendeleo iliyoandaliwa katika mpango wa shule.

4.3.2 Kuhamishia fedha katika halmashauri

Mpango utatumia mfumo wa serikali uliopo kutoa fedha kwa wakati. Kwa elimu ya msingi, fedha zitatolewa kupitia Akaunti Na. 5 kwenda kwenye akaunti za benki za shule. Mfuko/fedha za msaada kwa halmashauri zitatolewa katika Akaunti Na. 5. Fedha zitatolewa baada ya kutimiza masharti mengi kama itavyoelezwa zaidi hapo chini.

Fedha zitatolewa baada ya Mhasibu Mkuu kupokea idhini kutoka kwa BEDC ikiwa na yafuatyo:

- Majina ya halmashauri zinazotakiwa kupokea fedha.
- Kiasi kinachopaswa kulipwa kwa kila halmashauri.
- Maelezo kamili ya akaunti ya benki (Akaunti Na. 5) ambako fedha zitapelekwa (yaani jina la benki, mahali benki ilipo, aina ya akaunti na namba ya akaunti).
- Nakala ya kumbukumbu za BEDC zikiwa zimesainiwa na wajumbe wa kamati.
- Barua ya maelezo iliyoambatishwa, kutoka Ofisi ya Rais-TAMISEMI inayoomba kutolewa kwa fedha kuhusiana na utoaji fedha kwa ajili ya elimu ya msingi.

BEDC itaidhinisha kutolewa kwa fedha kutoka kwenye akaunti ya Benki Kuu ya Tanzania kwenda kwenye Mfuko wa Jumla na kuidhinisha orodha ya halmashauri zinazopaswa kupewa na kiasi kwa kila halmashauri. Kiasi kitakachotolewa kitakuwa sawa na kiasi kinachopaswa kutolewa.

Ofisi ya Rais-TAMISEMI itaandaa maombi kwa Mhasibu Mkuu kupeleka fedha zinazolingana na kiasi kilichoidhinishwa kwa ajili ya halmashauri katika Akaunti ya Wizara. Ofisa Mhasibu atahamisha fedha kutoka kwenye Akaunti ya Benki Kuu ya Tanzania na kuandaa taarifa ya Wizara ambayo kuzichukua fedha kwa ajili ya robo mwaka kwa kufuate kiasi kilichoidhinishwa na BEDC katika kasma ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI. Taarifa hii ya Wizara nakala yake hupelekwa Ofisi ya Rais-TAMISEMI.

Ofisi ya Rais-TAMISEMI itatuma vocha/hati ya malipo kwa kiasi kilichoidhinishwa kwa kila halmashauri kwa Ofisi Kuu ya Malipo (CPO) kwa ajili ya kuandaa TT (upelekaji fedha kwa njia ya simu) TT huandaliwa kwa ajili ya Akaunti ya Elimu ya halmashauri (akaunti Na. 5).

Baada ya kuipokea TT benki iliyo katika halmashauri husika itaifarifu halmashauri fedha zilizozingizwa katika akaunti Na. 5. Baada ya kuhakikisha katika Akaunti Na.5 kuwa fedha iliyoletwa imezingizwa kwenye akaunti, Mkurugenzi wa Halmashauri:

MWONGOZO WA MEMM WA HESABU NA USIMAMIZI WA FEDHA

- Ataandaa hati za benki za kutolea fedha au hundi kwa kadiri ya shule husika, na
- Atawateua walimu wakuu wa shule kuwa Maofisa Dhamana kwa ajili ya shule zao.


Kiasi kitakachoingizwa katika akaunti za benki za shule kitakuwa ni sawa kabisa na kile kilichoidhinishwa na BEDC.

4.3.3 Kuhamishia fedha katika shule

Halmashauri zitotoa fedha kwa shule kwa misingi ya ruzuku. Kiasi cha mwanzo kutolewa kwa shule kitakuwa kama kilivyo katika bajeti ya robo mwaka ya kwanza.

MWONGOZO WA MEMM WA HESABU NA USIMAMIZI WA FEDHA

MUHTASARI WA TARATIBU ZA KUHAMISHA NA KUSIMAMIA MFUKO WA MEMM



SC= Kamati za shule; BEDC = Kmaati ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi; RS = Sekretariati ya Mkoa

MWONGOZO WA MEMM WA HESABU NA USIMAMIZI WA FEDHA

*Kiongozi cha Halmashauri na shule kitatayarishwa ili kuharakisha na kurahisisha taratibu zilizopendekezwa katika mwongozo. Kiongozi hicho kitatumia viongozi vilivyopo vilivyoandaliwa kwa mujibu zinazoendelea kuhusu elimu katika halmashauri za shule.

5. SERA NA MIFUMO YA HESABU

5.1 SERA ZA HESABU ZA PROGRAMU

5.1.1 Maelezo ya Jumla

Sera ni mawazo mapana ambayo hujenga msingi wa maandalizi ya taarifa za fedha. Sera zilizotajwa hapa chini zinasisitiza juu ya matumizi ya sera zilizopo za hesbu za serikali ambazo hutumika katika IFMS (mfumo uliomo katika kompyuta) kwenye makao makuu ya wizara mbalimbali na mifumo iliyomo katika hali ya kompyuta na ile ya kuandikwa kwa mkono ya halmashauri na shule.

5.1.2 Kanuni za hesabu

Hesabu za MEMM hufuata kanuni na maelekezo ya taratibu za fedha za serikali kuu na serikali za mitaa kama zinavyorekebisha kila wakati na Wizara ya Fedha na Ofisi ya Rais-TAMISEMI.

5.1.3 Msingi wa hesabu

Programu itatumia msingi wa hesabu za fedha ambao hutumika na serikali huu na ambao unafaa kutumika katika ruzuku kubwa inayopelekwa katika halmashauri. Programu inaweza kubadili na kutumia aina nyingine ya hesabu kama msingi wa hesabu wa accrual iwapo serikali itaamua kuchukua mwelekeo huo hapo baadae.

5.1.4 Mapato ya Programu

Mapato ya Programu yatajumuisha kiasi halisi kilichochangiwa na wanajumuia, halmashauri, serikali kuu na wahisani wabia kwa madhumuni hayo. Mapato hayo yatajumuisha fedha:

- i. Zilizowekwa moja kwa moja katika Akaunti ya mfuko wa jumla
- ii. Zile zilizochangiwa kupitia akaunti ya mfuko wa MEMM
- iii. Fedha nyingine za wahisani
- iv. Zile zilioingizwa katika Akaunti Na. 5 na halmashauri zenyewe.

5.1.5 Matumizi yatakayogharimiwa na programu

Ni matumizi yanayostahiki na yaliyoidhinishwa kuhusiana na shughuli za programu tu ndiyo yatakayolipwa kwa kutumia akaunti ya programu.

5.1.6 Raslimali za kudumu na vifaa vya matumizi ya kawaida

Raslimali za kudumu, vitabu na vifaa vya stoo kwa matumizi ya kawaida vitanunuliwa na kutolewa maelezo kufuatana na Taratibu za Stoo za serikali zikiwa na nyongeza ya taratibu nyingine zozote zilizokubaliwa na wabia wanaoshiriki katika mfuko wa fedha na MEMM.

MWONGOZO WA MEMM WA HESABU NA USIMAMIZI WA FEDHA

Sera za nyongeza zifuatazo zitatumika kuhusiana na vifaa vitakavyopatikana kupitia programu hii:

- a. Raslimali zitakazopatikana kupitia programu hii zitathaminiwa gharama yake kama zilivyokuwa kabla ya kuanza kutumika na kutolewa maelezo chini ya kichwa cha habari cha kipengele kinachohusika kwenye matumizi.
- b. Vitabu vitachukuliwa kuwa ni raslimali inayohamishika na patakuwepo na daftari la kuvifanyia usajili ili kuwezesha kuvifanyia udhibiti mwishoni mwa mwaka au katika kipindi chochote itakapoonekana ni muhimu kufanya hivyo.
- c. Vitu vya matumizi visivyo vya kudumu vitagharimiwa katika mwaka wa ununuzi lakini kumbukumbu sahihi za vitu vya namna hiyo ambavyo vimesalia lazima zitunzwe.

5.2 MIFUMO YA HESABU NA TARATIBU

5.2.1 Akaunti inayomilikiwa katika Benki kuu ya Tanzania

Fedha zilizo katika Akaunti miliki ni mali ya Serikali ya Tanzania. Fedha hizi zinafanywa kuwa akaunti ya benki katika akaunti za serikali kwa kutumwa mfumo wa IFMS na kudhibitiwa na kuandikiwa taarifa kupitia mfumo huu. Mhasibu Mkuu atatoa taarifa zifuatazo kwa BEDC kutokana na data zilizomo katika mfumo, kwa kila robo mwaka:

- Mapato na malipo yaliyofanywa katika akaunti miliki ya MEMM ikionyesha undani wa miamala iliyofanywa kwa robo mwaka hiyo. Mapato yaonyesha chanzo cha fedha, malipo yaliyotolewa kutoka katika akaunti na baki ya fedha mwishoni mwa robo hiyo. Ripoti isambazwe kwa maofisa Uhasibu na BEDC.
- Maelezo ya malinganisho ya hesabu za benki ya akaunti miliki ya MEMM
- BoT itatoa ripoti za robo mwaka za ukaguzi wa ndani uliofanywa katika Akaunti miliki ya MEMM.

5.2.2 Katika Wizara ya Elimu na Utamaduni na Wizara Kuu

Miamala yote itatolewa maelezo kwa kutumia mifumo ya kawaida ya Serikali ya Tanzania kama ilivyo katika taratibu za Fedha, Maelekezo na Mwongozo wa IFMS.

Ni wajibu wa Wahasibu Wakuu katika Wizara ya Elimu na Utamaduni/au Ofisi ya Rais-TAMISEMI kuhakikisha kwamba Mhasibu Mkuu anatoa vificho vya akaunti kwa kufuata mfumo wa IFMS ili kuweka kumbukumbu za mikakati yote, maradi, mhisani na undani wa kila shughuli unaotakiwa kwa ajili ya menejimenti ya MEMM.

MWONGOZO WA MEMM WA HESABU NA USIMAMIZI WA FEDHA

Sehemu ya 1	Sehemu ya 2		Sehemu ya 3	Sehemu ya 4
Kasma, Programu, Programu ndogo	Kituo cha gharama	utekelezaji tarehe	Eneo la kijiografia	Takwimu za fedha za serikali (GFs) Alama ya kipengee
Wizara, Idara na Kitengo	Marekebisho ya sekta ya elimu, mgharamiaji, kituo cha gharama.	Mkakati, lengo na shughuli	Mkoa na halmashauri shughuli zinazogharamiwa	Uchambuzi wa kudhaminia kama gharama za usafiri.

5.2.3 Taratibu za hesabu katika halmashauri

Taratibu za hesabu katika halmashauri zitafuliwa matakwa ya sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Memorandumu ya Fedha ya Mamlaka za Mitaa, Mwongozo wa mahesabu wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa na taratibu na nyaraka zitakazotokana na hizo.

Pale itakapoonekana inafaa miundo ya vificho kama ilivyowekwa hapo juu kwenye serikali kuu inaweza kutumika.

5.2.4 Taratibu za malipo katika ngazi ya shule za msingi

5.2.4.1 Mapato

Mapato yote yatahifadhiwa benki katika akaunti ya shule. Mweka hazina wa shule atakuwa na kitabu cha fedha ambamo mapato yote yataingizwa.

Mweka hazina wa shule atatoa risiti kwa kila fedha iliyopokelewa ambapo nakala halisi atapelewa mlipaji, nakala moja itapelekwa kwa ofisa mwenye dhamana kila baada ya robo mwaka na nakala moja itabaki shuleni.

5.2.4.2 Taratibu za ulipaji za shule katika kutoa malipo shule zitazingatia taratibu zifuatazo:

- Malipo yanaidhinishwa vizuri yaani fedha za kutosha ziwepo kutosheleza matumizi baada ya kufikiria majukumu yaliyopo.
- Mwalimu mkuu wa shule (ofisa aliyeidhinishwa) ataidhinisha malipo kwa kuzingatia madai ya malipo yaliyokubaliwa hadi kiasi kilichopo na kwa madhumuni yaliyoonyeshwa kwenye Taarifa ya Wizara/Mkurugenzi mwidhinishaji wa Halmashauri.

Vocha ya malipo (ikiwa katika nakala tatu) itaandaliwa kwa ajili ya mgawaji/mtoaaji. Vocha za malipo zitafanyiwa kazi iwapo tu zipo fedha za kutosha katika kificho kinachohusika ambazo hazijapangiwa matumizi/majukumu. Ofisa mwidhinishaji anawajibika katika kuhakikisha kwamba maandalizi ya vocha za malipo yapo katika hali inayotakiwa. Halmashauri zitachapisha vitabu vya vocha za malipo kwa ajili ya matumizi ya shule.

MWONGOZO WA MEMM WA HESABU NA USIMAMIZI WA FEDHA

- Mweka hazina wa shule atatoa risiti kwa fedha yoyote iliyopokelewa ambapo nakala halisi atapelewa mlipaji, nakala moja itapelekwa kwa ofisa mwenye dhamana baada ya robo mwaka na nakala moja itabaki shuleni.
- Malipo yote yatafanywa kwa njia ya hundi au kuhamishiwa benki.

Malipo yanayohusu gharama za ugawaji/utoaji zitapaswa kuegemezwa/kuambatishwa na vifutavyo:

- Nakala ya Agizo la kununua ambalo itaambatana na Ankara ya mgawaji/mtoaaji
- Nakala hliisi ya Ankara ya mgawaji/mtoaaji
- Maelezo ya Bidhaa zilizopokelwa/hati ya kupokea bidhaa
- Hati ya kuwasilisha.

Ofisa aliyeidhinishwa au mtu mwingine aliyeteuliwa naye atahakikisha usahihi wa nyaraka kabla ya kuandikwa vocha ya malipo.

Mweka hazina wa shule (ambaye huteuliwa na kamati ya shule) ataandika vocha ya malipo na kuifikisha kwa Ofisa aliyeidhinishwa (ambaye anaweza asiwe ndiye mweka hazina) kwa ajili ya kutiwa saina.

